

Tathmini ya Hatua za Tafsiri kama Nyenzo ya Ufanisi wa Mawasilino

Hadija Jilala

Ikisiri

Makala haya yanahusu tathmini ya hatua za tafsiri kama nyenzo ya ufanisi wa mawasiliano. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uzalishaji wa tafsiri bora na sadifu yenye ushikamani wa maana na ujumbe wa matini chanzi katika matini lengwa. Makala haya yanajadili kwamba, endapo mfasiri hatafuata hatua thabiti za tafsiri anaweza kuzalisha tafsiri iliyokengeuka katika maana na ujumbe. Kwa hiyo, lengo la makala haya ni kupima utendekaji wa hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala (2014) katika modeli yake ya MMK¹ ili kuonesha namna hatua hizo zinavyoweza kutumika katika muktadha halisi wa zoezi la mchakato wa tafsiri. Katika kujadili jinsi hatua hizo zinavyotumika kutafsiri matini za kitamaduni, makala haya yanapima ufaavu wa hatua hizo kama mwongozo wa kutafsiri matini za aina zingine. Makala haya yanajadili kuwa hatua hizo zinaweza kutumika kama mwongozo wa kutafsiri matini za aina nyingine na ni nyenzo madhubuti ya kufikia ufanisi wa mawasiliano kwa jamii za lugha tofauti. Tafsiri yoyote haiwezi kuwa sadifu kama mfasiri hatazingatia hatua muafaka za kutafsiri. Kwa maana hiyo, hatua za tafsiri ni kipengele muhimu katika kuwasilisha maana na ujumbe sadifu wa matini chanzi katika matini lengwa ili kufanikisha mawasiliano.

1.0 Utangulizi

Tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo na ujumbe wa maandishi kutoka katika lugha ya utamaduni mmoja kwenda katika lugha ya utamaduni mwingine (Catford, 1965; Katani, 1999; Munday, 2001; Venuti, 2002; Wang, 2008). Tafsiri kama zoezi ni mchakato ambao huhitaji kufanywa kwa maarifa, stadi, ujuzi, uzoefu, weledi na maarifa ya nadharia na vitendo. Mbali ya kuelewa nadharia mchakato huu, kama utendaji, huhitaji kufanywa kwa ufanisi wa hali ya juu ili kuepuka mianya ya upotoshaji wa maana na ujumbe wa matini iliyokusudiwa. Kwa maana hiyo, ni mchakato ambao unahitaji kuwekewa misingi thabiti ya

¹ Modeli ya Mawasiliano ya Kitamaduni ambayo ilipendekezwa na Jilala (2014) kama mwongozo wa kinadharia wa kutafsiri matini za kitamaduni. Katika modeli hii, hatua za tafsiri ni moja ya kijenzi cha modeli ambazo zilipendekezwa kama hatua za kutafsiri matini za kitamaduni baada ya data za utafiti kudhihirisha kuwa hatua zilizopendekezwa an Newmark (1988) na baadaye Mwansoko (1996) kujikita katika ujumla na kuonekana zinakwama katika kutafsiri matini za kitamaduni.

kinadharia na vitendo. Moja ya misingi thabiti ni uzingativu wa hatua za tafsiri wakati wa mchakato mzima wa kutafsiri. Tafsiri kama mchakato huhitaji kuwepo kwa hatua zilizopangwa kimantiki ili kuweza kufikia ufanisi wa mawasiliano. Hatua hizi ndiyo dira maalumu inayomuongoza mfasiri kujiandaa kisaikolojia juu ya zoezi la tafsiri. Kwa maana hiyo, hatua za tafsiri ndiyo msingi wa awali ambao mfasiri anatakiwa kuzingatia kabla ya kuanza kufanya kazi ya tafsiri.

Tunapozungumzia hatua za tafsiri tunarejelea ule mfuatano wa matukio ambayo mfasiri hupitia ili kuzalisha matini ya tafsiri (Newmark, 1988; Mwansoko, 1996; Nida, 1969). Ni mwongozo na dira maalumu inayomwongoza mfasiri katika kutekeleza zoezi la mchakato wa kutafsiri matini. Aidha, kwa kuzingatia hatua zilizowekwa, mfasiri huweza kujua ni mambo gani ya msingi anapaswa kuzingatia anapoukabili mchakato wa kutafsiri. Katika mchakato wa tafsiri kuna hatua kuu tatu ambazo mfasiri anatakiwa kufuata katika kuoanisha hatua za tafsiri na mchakato mzima wa tafsiri. Hatua hizo kuu ni; kabla ya zoezi, wakati wa zoezi na baada ya zoezi la kutafsiri. Katika hatua hizo, mfasiri anatakiwa kuwa makini na kuzingatia mambo mahususi wakati akifikiria kufanya zoezi la tafsiri. Kwa hiyo, hatua za tafsiri ni kipengele muhimu sana ambacho huweza kuleta athari ama chanya au hasi katika zoezi la tafsiri. Hatua za tafsiri kama mwongozo wa vitendo katika tafsiri zina manufaa na umuhimu ufuatao katika zoezi la tafsiri

- (i) Ni dira ambayo humsaidia mfasiri kuweza kuzikabili matini kwa kufuata hatua mahususi.
- (ii) Humsaidia mfasiri kuelewa maudhui/ujumbe wa matini chanzi ambao anahitaji kuhawilishwa katika matini lengwa.
- (iii) Humsaidia kubaini lengo la tafsiri na lengo la matini asilia.
- (iv) Humsaidia mfasiri kubaini na kuteua nadharia ya tafsiri itakayomuongoza katika zoezi hilo.
- (v) Humsaidia kubaini na kuteua mbinu muafaka ya kutafsiri matini aliyonayo.
- (vi) Humsaidia kuzalisha matini bora ya tafsiri yenye maana na ujumbe sadifu.

Kama tulivyoona hapo juu hatua za tafsiri ni kiini cha zoezi la tafsiri ambacho hujumuisha maarifa ya nadharia na vitendo katika mchakato mzima wa zoezi hilo.

Kwa maana hiyo basi, tafsiri kama mchakato unaotumia nadharia na vitendo, hutegemea kuwepo kwa hatua ambazo zitaongoza zoezi la uhawilishaji wa mawazo na ujumbe kutoka katika lugha moja kwenda katika lugha nyingine. Hata hivyo, endapo mfasiri atashindwa kufuata hatua mahususi katika zoezi hilo anaweza kuzalisha tafsiri yenye ukengeufu wa maana na ujumbe. Kwa hiyo, kuna haja ya kuchunguza na kufanya tathimini ya hatua za tafsiri kama nyenzo muhimu ya kufikia ufanisi wa mawasiliano. Katika kufikia hilo makala haya yanafanya tathimini na kujadili hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala (2014) kama

mwongozo wa kutafsiri matini za kitamaduni katika modeli yake ya MMK iliyotokana na data za utafiti wa uzamivu. Katika utafiti huo, mtafiti hakulenga kufanya tathimini ya hatua alizopendekeza kutokana na data alizozipata.

Aidha, hakuwa na lengo la kuona kama hatua hizo zinaweza kutumika katika kutafsiri matini za aina nyingine. Kwa maana hiyo basi, makala haya yanafanya tathimini ya hatua za tafsiri kama nyenzo muhimu ya mawasiliano na kupima ufaavu wa hatua hizo katika kutafsiri matini nyingine tofauti na matini za kitamaduni. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kubaini endapo hatua hizi zinafaa kutumika kama dira ya kutafsiri matini za aina nyingine au kufanya marekebisho kidogo. Katika kujenga mjadala huo, makala yanaonesha namna mfasiri anavyoweza kutumia hatua hizo katika kutafsiri matini za kitamaduni na pia kudhihirisha uthabiti wake kama dira ya mchakato wa tafsiri. Swali la msingi ambalo lilitoa msukumo wa kufanya tathimini ya hatua za tafsiri ni kwamba; je mfasiri wa matini za kitamaduni anawezaje kuzitumia hatua zilizopendekezwa na Jilala katika MMK? Je hatua hizo zinaweza kutumika kama dira ya kutafsiri aina nyingine za matini kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza au kinyume chake? Katika kujibu maswali hayo makala haya yamejikita katika data za matini za kitalii zilizotafsiriwa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza ili kupima uthabiti wa hatua hizo kama nyenzo maalumu ya kufanikisha mawasiliano.

2.0 Aina za Matini

Tunapozungumzia aina ya matini tunarejelea uainishaji wa matini za tafsiri. Wataalamu mbalimbali wamebainisha aina za matini kulingana na mikabala wanayotumia katika kuainisha matini hizo. Kwa mfano, Mwansoko (1996) anapendekeza uainishaji wa matini kwa kutumia dhima za lugha za Bühler (1965), wazo ambalo pia lilipendekezwa na Newmark (1988). Kwa kuzingatia dhima za lugha Mwansoko (1996) amebainisha matini zifuatazo:

- (i) *Matini elezi*: ni zile zinazoegemea kwa mwandishi na mwandishi hutumia lugha kuelezea hisia zake bila kujali hadhira itapokea vipi. Mfano wa matini elezi ni kazi za kifasihi kama vile ushairi, hadithi fupi, tamthiliya na riwaya; kauli za kimamlaka au kimadaraka kama vile, hotuba na nyaraka za kisiasa, nyaraka za kisheria, kazi za sayansi, falsafa na kitaaluma; na wasifu nafsi, insha na mawasiliano ya kibinafsi baina ya watu.
- (ii) *Matini arifu*: ni matini zinazohusu mada yoyote ile ya maarifa, mfano sayansi, teknolojia, biashara na uchumi. Aina hii ya matini huwa katika maumbo sanifu, mathalani vitabu, ripoti za kiufundi, makala katika magazeti au majarida ya kitaaluma, tasnifu na madondoo ya ajenda au kumbukumbu za mikutano.
- (iii) *Matini amili*: hizi hujumuisha matini zote zinazoegemea zaidi upande wa hadhira, yaani wasomaji. Hulenga kuibua hisia za msomaji na kumfanya

afikiri au atende kwa namna ambayo imekusudiwa na matini mahususi kwa mfano, matangazo, maelekezo, propaganda, maombi, mialiko na fasihi pendwa.

Pamoja na mkabala huo wa uainishaji wa matini tuliouona hapo juu. Mwansoko (1996) pia ameinisha matini kwa kuzingatia namna matini zinavyotumia istilahi au msamiati wa kiufundi. Kwa kutumia kigezo hicho, ameinisha aina tatu za matini, ambazo ni matini za kiufundi ambazo hutumia kiwango kikubwa cha istilahi; matini za nusu-kiufundi ambazo hutumia istilahi chache, na matini zisizo za kiufundi, ambazo hazitumii istilahi bali msamiati wa kawaida.

Mjadala wa makala haya umejiegemeza katika uainishaji wa matini kulingana na utumiaji wa istilahi au msamiati uliofanywa na Mwansoko (1996). Uainishaji huu wa matini unatuongoza katika kufanya tathmini ya hatua za tafsiri na kupima ufaavu wake kama nyenzo ya ufanisi wa mawasiliano kwa jamii zenye za utamaduni tofauti.

3.0 Hatua za Tafsiri

Hatua za tafsiri, kama moja ya vipengele muhimu vinavyohitaji kuzingatiwa katika tafsiri, kimejadiliwa na wataalamu mbalimbali wa tafsiri. Newmark (1988) amependekeza hatua saba za kuzingatia katika kufanya tafsiri. Akikubaliana na Newmark, Mwansoko (1996: 19-23) naye amekubali kuwa kuna hatua saba za kufuata katika mchakato wa tafsiri. Hatua hizo ni (i) maandalizi, (ii) uchambuzi, (iii) uhawilishaji, (iv) usawidi wa rasimu ya kwanza ya tafsiri (v), udurusu wa rasimu ya kwanza ya tafsiri, (vi) usomaji wa rasimu ya tafsiri na mtu wa pili na (vii) usawidi wa rasimu ya mwisho ya tafsiri. Lakini, Jilala (2014) anadai kuwa, hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Newmark (1988) na Mwansoko (1996) haziwezi kutumika katika kutafsiri matini za kitamaduni, hususani katika jamii ulumbi, kama Tanzania. Anaendelea kusesitiza kuwa, katika jamii ulumbi, matini za kitamaduni zinahitaji hatua mahususi ili kuhawilisha maana na ujumbe linganifu wa kitamaduni kwa sababu ya mtawanyiko wa kitamaduni. Katika tathmini ya hatua za tafsiri, Jilala anahitimisha kuwa, hatua zilizopendekezwa na Mwansoko ni za jumla kiasi kwamba zinaweza zisimfikishe mfasiri katika lengo la tafsiri ya matini za kitamaduni. Katika hitimisho lake, Jilala anapendekeza hatua tano za kuzingatia wakati wa kufanya mchakato wa kutafsiri matini za kitamaduni. Katika makala haya tunajadili namna mfasiri anavyoweza kuzifuata hatua hizo ili kufanikisha mawasiliano na pia kupima ufaavu wa hatua hizo katika kutafsiri matini za aina nyingine. Kwa kufanya hivyo tutaweza kubaini endapo hatua hizo zimejikita katika matini mahususi au zinaweza kutumika kutafsiri matini nyingine na kuwa mbadala wa uboreshaji wa hatua zilizopendekezwa na Mwansoko (1996).

4.0 Hatua za Tafsiri katika Matini Mahususi

Tumekwishaona hatua za tafsiri za matini zilizobainishwa na Newmark (1988) na kuungwa mkono na Mwansoko (1996). Kwa upande mwingine, Beaton *na wenzie* (2002) wanapendekeza hatua tatu za kutafsiri matini za kitamaduni, nazo ni; kutambua uhusiano au muktadha wa lugha, kupima maana ya tafsiri ya neno katika lugha zote na kurudia mchakato mzima ili kupata ulinganifu katika tafsiri. Tofauti na Beaton *na wenzie*, katika kuchunguza hatua za kutafsiri matini za kitamaduni Jilala (2014) anadai kuwa, hatua za tafsiri mbali ya kutegemea aina ya matini, hutegemea na utamaduni wa lugha anazozishughulikia mfasiri wa matini. Anajadili kuwa, matini za kitamaduni hufuata hatua mahususi za tafsiri. Katika modeli yake Modeli ya Mawasiliano ya Kitamaduni (MMK), Jilala anapendekeza hatua tano mahususi ambazo zinafaa kutumika katika mchakato wa kutafsiri. Hii ina maana kwamba, mfasiri hutegema aina ya matini anayokusudia kutafsiri ili kuamua ni hatua gani azifuate. Kwa mfano, mtu anayetafsiri matini zenye misamiati ya kawaida, hahitaji kuchunguza maana ya neno la MC kwenye ML. Kwa hiyo, kamusi inatosha kumpa maana na ujumbe wa msamiati unaohusika. Kwa maana hiyo, kuna baadhi ya misamiati ambayo tayari kamusi zinatoa maana yake na inajulikana kwa jamii lengwa na jamii chanzi kwa mfano; *kikombe* 'cup,' *kijiko* 'spoon,' *sahani* 'plate,' *meza* 'table' *chumba* 'room' *kalamu* 'pen.' Misamiati hii ni maneno ya kawaida katika mawasiliano ya lugha. Ni dhahiri kwamba, maneno hayo huashiria kitu kilicho sawa katika jamiilugha ya Kiswahili na jamiilugha ya Kiingereza. Kwa upande mwingine, matini za kitamaduni huhitaji hatua mahususi ili kuweza kupata maana na ujumbe wake. Aidha, kwa vile matini za kitamaduni hueleweka ndani ya utamaduni mahususi ni dhahiri kwamba mfasiri anapaswa kufuata hatua mahususi za tafsiri ili kufikia lengo la mawasiliano.

Isitoshe, baadhi ya wafasiri hutafsiri matini bila kuzingatia hatua za tafsiri zilizopendekezwa na wataalamu wa tafsiri. Kwa mfano wakati wa kuchunguza hatua za tafsiri zinazotumiwa na wafasiri wa matini za kitalii, Jilala (2014) alibaini kuwa, wafasiri hutumia mbinu tofauti na zile zilizobainishwa katika nadharia za tafsiri. Kwa hiyo, utendaji katika muktadha halisi wa tafsiri hutofautiana na nadharia zilizowekwa. Jedwali namba 1 hapa chini linaonyesha hatua amabzo hufuatwa na wafasiri wa matini za kitalii wakati wa kutafsiri matini za kitamaduni kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.²

² Data hii ilipatikana katika utafiti wa uzamivu uliofanywa na Jilala, 2014 wakati wa kuchunguza hatua za kutafsiri matini za kitamaduni.

Jedwali Na 1: Hatua za Kutafsiri Matini za Kitamaduni-Wafasiri wa Matini za Kitalii

Na.	Hatua za Kutafsiri Matini za Kitamaduni
1.	Kufanya utafiti wa maneno ya kitamaduni kwa makabila yanayohusika
2.	Kutafsiri maneno ya kitamaduni kwa kuhusisha jamii ya utamaduni wa jamiilugha inayohusika.
3.	Kutafuta neno la Kiswahili la neno la kitamaduni
4.	Kutafuta neno la Kiingereza
5.	Kuhakiki neno lililoteuliwa kutoka katika kamusi
6.	Kuisoma matini kwa kuwashirikisha wafanyakazi wengine
7.	Kulinganisha tafsiri ya neno katika tafsiri moja na nyingine

Chanzo: Data za matini za kitalii (Mei –Oktoba, 2012)

Jedwali Na. 1, linaonesha hatua za kutafsiri matini za kitamaduni zilizobainishwa na wafasiri wa matini za kitalii. Kama ilivyokwishaelezwa, hatua hizi zinatofautiana na hatua zilizopendekezwa na Newmark (1988) na Mwansoko (1996). Tofauti hii inadhihirisha kuwa, kuna tofauti baina ya nadharia za tafsiri na utendaji katika muktadha halisi. Hatua zinazotajwa katika nadharia zinatofautiana na zile zinazotumika katika muktadha halisi wa mchakato wa kutafsiri. Hii ina maana kwamba, si hatua zote zilizopendekezwa na wataalam wa tafsiri zinatumiwa katika uhalisia wa kutafsiri. Bali mfasiri huamua ni hatua zipi azitumie kulingana na muktadha wa matini aliyo nayo (Vermeer, 1989). Pamoja na tofauti hii lakini bado tunaona kwamba mfasiri anahitaji kufuata hatua maalumu ili kuweza kutimiza lengo la tafsiri. Tafsiri si hadithi, bali ni mchakato unaohitaji mantiki katika utekelezaji wake.

Aidha, hatua za kutafsiri matini za kitamaduni zinatofautiana kwa sababu, hatua za kutafsiri hutegemea aina ya matini na muktadha wa kitamaduni. Kwa mfano, ukichukulia hatua ambazo zilipendekezwa na Newmark (1988) na Mwansoko (1996) utaona kuwa ni hatua za jumla katika mchakato wa tafsiri na haziwezi kutumika kutafsiri matini maalumu, hususani matini za kitamaduni kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Tanzania ni jamii ulumbi ambayo kulingana na muktadha wa kitamaduni, inaonesha kuwa kuna mtawanyiko wa kitamaduni ambao hutokana na kuwepo kwa lugha za kijamii zaidi ya 120 zenye kaida, mila, desturi, miiko na kanuni zake mahususi ambazo hutofautiana baina ya jamiilugha moja na nyingine. Kwa mfano, Mmasai anapotaja ‘ng’ombe’ kwake anapata maana mbalimbali tofauti na Mzanaki anapotaja ‘ng’ombe.’ Kama ilivyoonekana katika matini za kitalii, tamaduni hizi huelezewa na kuwasilishwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo hutumika kama daraja la mawasiliano.

Jilala (2014) anadai kuwa, katika muktadha wa jamii ulumbi kama Tanzania, baadhi ya hatua ambazo zimependekezwa na wataalamu wa tafsiri hazitoshelezi katika kutafsiri matini za kitamaduni. Aidha, kutokana na matokeo ya data za utafiti, alipendekaza hatua tano za kuzingatia wakati wa kutafsiri matini za kitamaduni ili kufikia ufanisi wa mawasiliano ya kitamaduni. Hatua hizi zinaweza kukabiliana na muktadha wa mtawanyiko wa kitamaduni na changamoto zake. Hatua zilizopendekazwa na Jilala (2014:) ni kama zinavyojidhihirisha katika jedwali namba 2:

Jedwali Na 2: Hatua za Kutafsiri Matini za Kitamaduni

Na.	Hatua	Vipengele vya Kuzingatia.
I.	Maandalizi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchambua maudhui ya matini • Kubainisha maneno ya kitamaduni • Kubaini ujumbe na maana ya maneno • Kubaini lengo la MC³ na ML⁴
II.	Utafutaji wa visawe vya kitamaduni	<ul style="list-style-type: none"> • Ushirikishaji wa jamii za UC⁵ na UL⁶. • Kuhakiki visawe vya UC na UL.
III.	Mchakato wa tafsiri	<ul style="list-style-type: none"> • Kupima ulinganifu wa visawe vya kitamaduni katika MC na ML • Kupima ushikamani wa matini ya UC na UL.
IV.	Uhusiano	<ul style="list-style-type: none"> • Kupima kufanana kwa dhana, ishara na ujumbe wa UC na UL • Kupima uhusiano wa ujumbe wa UC na UL katika MC na ML
V.	Uzalishaji wa ML	<ul style="list-style-type: none"> • Uhariri • Ushirikishaji wa hadhira ya UC na UL • Ushirikishaji wa wataalam wa lugha na tafsiri • Udurusu wa rasimu ya kwanza • Usawidi wa rasimu ya mwisho

Chanzo: Jilala, 2014:

Jedwali Na. 2 linaonesha hatua tano za kutafsiri matini za kitamaduni ambazo ni; maandalizi, utafutaji wa visawe vya kitamaduni, mchakato wa tafsiri, uhusiano na uzalishaji wa matini lengwa. Hatua hizi zinatofautiana na zile zilizobainishwa na

³ Matini chanzi

⁴ Matini lengwa

⁵ Utamaduni chanzi

⁶ Utamaduni lengwa

wataalamu wengine wa tafsiri ingawa baadhi ya vipengele katika hatua hizo vimetokana na hatua za Mawansoko (1996). Kwa maana hiyo, hatua hizi zimetokana na mawazo ya wataalamu na matokeo ya data za utafiti.

Baada ya kuziwasilisha hatua za tafsiri, sehemu inayofuta inajadili jinsi hatua hizo zinavyoweza kutumiwa na mfasiri katika mchakato wa kutafsiri. Ikumbukwe kuwa, hatua hizi zinaanza kufanya kazi kabla, wakati na baada ya kuzalisha kazi ya tafsiri. Kwa maana hiyo, mfasiri anapopata kazi ya kutafsiri anapaswa kujiandaa kisaikolojia kwa kujua wajibu na jukumu lake katika matini hizo. Mfasiri lazima afahamu aina ya matini anayoikabili na pia ajue ni lugha zipi anazozifanyia kazi. Sambamba na matayarisho hayo ya kisaikolojia, mfasiri anahitaji kutambua muktadha na mazingira yanayomzunguka. Je, kuna vifaa vya kutosha katika kuifanya kazi ya tafsiri? Vifaa ni pamoja na kamusi za lugha zote anazozifanyia kazi, kamusi za lugha moja na lugha mbili, kalamu, daftari na rangi. Mfasiri pia anahitaji kuandaa mazingira rafiki ambayo yatampa usikivu na utulivu wakati wa shughuli nzima ya tafsiri.

Katika sehemu ifuatayo unajadili namna hatua za tafsiri zinavyoweza kutekelezeka kwa vitendo katika muktadha halisi wa kutafsiri matini za kitamaduni.

4.1 Maandalizi

Hii ni hatua ambayo mfasiri wa matini yoyote lazima aizingatie. Katika hatua ya maandalizi mfasiri anapaswa kuwa na matini anazozifanyia kazi na kutambua lugha anazotakiwa kuzitumia katika matini hizo. Hii ina maana kwamba, mfasiri hapa anajiandaa kisaikolojia kwamba ana matini anazohitaji kutafsiri yaani MC na ML, na lugha anazotakiwa kuzifanyia kazi. Katika hatua hii, kuna maswali ya msingi ambayo mfasiri anapaswa kujiuliza nayo ni; Je matini chanzi ni ya lugha gani? Je matini lengwa inatakiwa kuwa katika lugha gani? Na je, nina vifaa vya kutosha kuzikabili matini hizi? Je nina ujuzi wa kutosha wa lugha na utamaduni wa lugha hizi? Je kuna watu ambao wanaweza kunisaidia kunipa data za matini hizi endapo nitakwama? Je mazingira yangu ni rafiki katika kufanya kazi hii? Maswali haya humsaidia mfasiri kuweza kujiamini na kuamini kuwa atakuwa mwaminifu kwa matini zote mbili. Vermeer (*keshatajwa*) anasema kuwa, mfasiri wa matini lazima awe na weledi wa lugha na utamaduni wa jamii kabla ya kutafsiri matini. Mjadala huu pia unasisitizwa na Jilala (2014) ambaye anadai kuwa, tafsiri ya matini za kitalii kutoka Kiswahili kwenda Kingereza zina mapungufu ya kimawasiliano kwa sababu zimetafsiriwa na wafasiri ambao hawana weledi wa lugha na taaluma ya tafsiri. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwa mfasiri kufanya tathimini binafsi juu ya weledi wake na ujuzi alionao katika lugha zote mbili na tamaduni za lugha hizo. Pia, kufanya tathimini binafsi juu ya ujuzi katika maarifa, nadharia na uzoovu wa kutafsiri. Kwa mfano, mfasiri anapokutana

na matini ya sheria ya ndoa inayohitaji kutafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili. Tazama mifano ifuatayo:

1. “in their marriage they have two issues”.

Hapa mfasiri anajianda kuwa anashughulikia lugha mbili Kiingereza ambayo ni lugha Chanzi (LC) na Kiswahili ambayo ni lugha lengwa (LL).

2. Amina umejitenga kufa umetangulia, kama ua umefunga baada ya kuchanua

Katika mfano namba 2. Mfasiri anatambua kuwa ana matini ya Kiswahili (MC) na Kiingereza (ML). hii ina maana kwamba anajiandaa katika lugha na tamaduni za lugha hizo.

Maandalizi ya awali ambayo huambatana na saikolojia ya kuipokea kazi na kuandaa mazingira ya namna ya kukabiliana na kazi hiyo, mfasiri anapokuwa tayari sasa kuikabili kazi lazima afanye shughuli mbalimbali katika maandalizi hayo. Sehemu zifuatazo ni miongoni wa maandalizi mahususi ambayo mfasiri anatakiwa kuyafanya wakati akijiandaa kufanya tafsiri.

4.1.1 Kuchambua Maudhui ya Matini

Katika kipengele hiki, mfasiri anahitaji kuchambua maudhui ya matini anayoikusudia. Uchambuzi wa matini chanzi huanza kwa kusoma matini yote na kuielewa ili kuweza kubaini maudhui ya matini chanzi. Zoezi la uchambuzi wa maudhui ya matini huongozwa na maswali kadhaa ambayo yatamsaidia kuibua maudhui ya matini iliyopo mbele yake. Maswali hayo ni; Je, maudhui ya matini haya ni nini? Nini lengo la mtunzi asilia wa matini chanzi? Je matini chanzi ina maana na ujumbe gani? Je lengo la mfasiri ni lipi? Je lengo la matini lengwa ni lipi? Je, neno ama msamiati huu ameutumia kwa maana gani? Je umetumika kama sitiari ama ishara (kama ni matini ya kifasihi). Kwa kujiuliza maswali hayo, mfasiri anaweza kuibua maudhui ya matini chanzi na kuwa tayari kuyahamisha maudhui hayo katika lugha lengwa. Ikiwa msamiati wa matini chanzi umetumika kama sitiari ama tashibiha, ishara, ama tashihisi, wajibu wa mfasiri ni kutafuta sitiari katika utamaduni lengwa inayowasilisha ujumbe uliosawa na sitiari ya matini chanzi. Kwa ujumla, matini chanzi huwa na maneno makuu ambayo yanabeba maana, ujumbe na maudhui ya matini hiyo (Hosseini, 2008). Kwa hiyo, mfasiri anatakiwa kuyabainisha maneno hayo ili kuweza kuyatafutia visawe vyake katika lugha lengwa kabla ya zoezi la tafsiri.

Kubainisha maneno yenye sifa amilifu hapa mfasiri anahitaji kubainisha maneno yote yenye sifa amilifu. Kwa mfano, msamiati wa kiufundi, msamiati wa kisayansi, msamiati wa kitamaduni ama tamathali za semi. Kwa kufanya hivi,

mfasiri huyaweka kando maneno na msamiati huo na kubaini nafasi ya msamiati huo katika ujenzi wa maana na ujumbe wa matini chanzi. Mfasiri anaweza kuyapigia mstari ama kuyaandika katika shajara kama maneno hayo yapo katika kifungu cha habari. Hatua hii inamsaidia mfasiri kuelewa endapo msamiati huo umebeba ujumbe na maudhui ya matini au la. Aidha, inamsaidia kujiandaa kujua misamiati ambayo ni ya kiufundi, nusu kiufundi ama si ya kiufundi katika matini yake. Kwa mfano, katika matini yetu ya awali mfano wa kwanza tumeona neno 'issue' na katika mfano wa pili wa matini ya Kiswahili kuna neno 'kujitenga,' 'ua,' 'umefunga' na 'kuchanua.' Kwa maana hiyo, mfasiri anatakiwa kubaini maana asilia, maana za ziada na maana za kimuktadha za maneno hayo.

Katika hatua hii mfasiri pia anahitaji kubaini hadhira lengwa na sifa zake je hadhira lengwa ni watalii, kiwango cha elimu, je ni watu wazima, vijana ama watoto. Mwansoko (1996:16) anasema ni vema mfasiri akatambua hadhira mahususi ya matini lengwa yake. Yafaa ajiulize: je msomaji wake ni yupi? Ana elimu, umri au jinsia gani? Yupo katika tabaka lipi la kijamii? Yu msomi wa kawaida au msomi aliyebobea? Majibu ya maswali haya yatamsaidia mfasiri kufanya uamuzi juu ya kiwango cha urasimi, mhemko pamoja na ugumu au usahili atakaopaswa kuzingatia wakati anafasiiri matini yake (Mwansoko, 1996). Ubainishaji wa hadhira lengwa utamsaidia katika uteuzi wa visawe na mbinu za kutafsiri matini aliyonayo.

Jambo jingine ambalo mfasiri wa matini ya kitamaduni anapaswa kuzingatia wakati wa uchambuzi wa maudhui ya matini ni kubaini mtindo na umbo la matini chanzi. Mfasiri anapaswa kuchunguza athari ya mtindo na umbo la matini chanzi katika kuwasilisha ujumbe na maana ya matini chanzi. Ni vema kuzingatia mtindo na umbo la matini chanzi ili kuweka ulinganifu wa matini hizo mbili.

4.1.2 Kubaini Ujumbe na Maana ya Maneno

Katika hatua hii mfasiri anatakiwa kubaini ujumbe na maana ya maneno aliyoyabaini katika matini chanzi. Kipengele hiki ni muhimu sana kwa sababu ndicho kitakachomwongoza katika kuelewa maana na ujumbe wa misamiati aliyobainisha ili aweze kuyahamishia mawazo hayo katika matini lengwa. Hatua hii huongozwa na maswali ya msingi katika ubainishaji wa maana na ujumbe wa maneno. Maswali hayo ni: Je maneno haya yamebeba maana gani? Je ni ujumbe gani ambao mwandishi asilia ameulenga? Kwa kupata maana na ujumbe wa MC itamsaidia kuhamisha ujumbe na maana ya maneno hayo katika ML. Tazama mifano katika jedwali namba 3.

Jedwali Na. 3: Ubainishaji wa Maana na Ujumbe

Na.	MC	Maana na Ujumbe katika MC
1.	Laiboni	?
2.	Ubusoka	?
3.	Mbegete	?

Chanzo: Data za matini za Kitalii

Mifano ya maneno katika jedwali namba 3 hapo juu inaonyesha jinsi mfasiri anavyoweza kubainisha maneno katika matini yake na kuyatafutia maana na ujumbe wake. Kwa hiyo, mfasiri anapaswa kuchunguza na kubaini maana na ujumbe wa maneno hayo katika utamaduni chanzi na pia kuchunguza iwapo maneno hayo yana maana katika jamii ya utamaduni lengwa. Vile vile, achunguze endapo ujumbe wa maneno hayo katika utamaduni wa MC ni sawa na ujumbe wa visawe vyake katika utamaduni wa ML. Kwa kuelewa maana na ujumbe wa maneno hayo, itamsaidia mfasiri kuamua ni mbinu gani atumie katika kutafsiri matini hizo. Vile vile, uelewa wa maana na ujumbe utamwongoza katika kuteua visawe vya maneno hayo katika utamaduni lengwa. Mfasiri ataweza kuteua visawe ambavyo vitasaidia kuhifadhi ulinganifu wa maana na ujumbe wa MC na ML.

4.1.3 Kubaini lengo la MC na ML

Kipengele hiki ni sehemu muhimu katika maandalizi. Mfasiri anapaswa kujua lengo mahususi la matini chanzi na matini lengwa. Ili kuibua lengo la matini mfasiri anajikita katika maswali ya msingi kama vile; Je, mwandishi wa matini chanzi alilenga nini katika matini yake? Je amekusudia nini kwa hadhira yake. Kwa hiyo, ubainishaji wa lengo utamsaidia mfasiri kuhamisha lengo hilo katika muktadha lengwa ili kusaidia hadhira lengwa kupata ujumbe lengwa uliokusudiwa sawia na hadhira chanzi. Kujua lengo la matini kutamsaidia msomaji wa matini kuelewa aina ya tafsiri anayotakiwa kuzalisha. Aidha, hatua hii itampa mfasiri uwezo wa kuteua visawe vya lugha lengwa ambavyo vina ulinganifu na matini chanzi ili kukidhi lengo la kutafsiri matini chanzi. Kwa mfano, endapo mfasiri atagundua lengo la matini chanzi ni kuwasilisha utamaduni wa jamii chanzi kwa jamii lengwa. Mfasiri anapaswa kufumbata lengo hilo, hata kama misamiati iliyotumika katika MUC haipo katika utamaduni lengwa. Endapo atabaini hilo, basi mfasiri itabidi atumie mbinu ya uasilishaji na ufafanuzi wa visawe kwa kuhamisha neno kama lilivyo kutoka katika MC kwenda katika ML na kisha kutoa ufafanuzi wa maana na ujumbe wa kitamaduni uliobebwa na neno/matini. Kwa mfano, katika uchunguzi wa tafsiri ya matini za kitalii iligundulika kuwa, lengo la kutafsiri matini za kitalii kutoka Kiswahili – Kiingereza ni kuweka wazi taarifa za utamaduni kwa watalii ili waweze kuelewa na kufahamu utamaduni wa jamii ya Tanzania (Jilala, 2014). Kutokana na lengo hilo, mfasiri wa matini chanzi alitegemewa kutimiza lengo hilo. Tazama mfano katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 4: Ubainishaji wa Matini za Kitamaduni

Na.	MC	Neno la Kitamaduni
1.	Mgonjwa aliyeshidikana hupelekwa katika kijumba cha Kinyamkera ⁷	Kinyamkera
2.	Wagonjwa hupelekwa katika kijumba cha shetani	Kijumba cha shetani
3.	Wazee hunywa Mbege	Mbege
4.	Alipofariki alizikwa akiwa amekaa kwenye Kigoda	Kigoda
5.	Jamii ya wamasai ina makundi mawili morani na laiboni	Morani Laiboni

Chanzo: Matini za Kitalii (2012)

Mifano katika jedwali namba 4 inonyesha maneno ambayo yamebeba ujumbe wa kitamaduni. Katika hatua hii, mfasiri atakuwa amebaini lengo la kutafsiri matini hizo. Kwa hivyo, baada ya mfasiri kubaini maneno hayo katika matini chanzi, anatafuta visawe vyake katika matini lengwa. Ikiwa maneno hayo hayamo katika utamaduni chanzi, yaani ni mageni na utamaduni lengwa hauna utamaduni huo, basi mfasiri huyatolea ufafanuzi ili kufikia lengo la tafsiri ambalo ni kufahamisha utamaduni chanzi kwa hadhira ya utamaduni lengwa. Kwa maana hiyo, mfasiri anahamisha maneno ya MC kama yalivyo katika ML na kuyafanyia ufafanuzi. Tazama mifano ifutayo katika jedwali namba 5;

Jedwali Na. 5: Mifano ya Tafsiri

Na.	MC	ML
1.	Kinyamkera	Kinyamkera (<i>small hut in Kwere society used as a special room to handle uncritical diseases</i>)
2.	Kijumba cha shetani	Kijumba cha shetani (<i>A small hut in Kwere society used as a special room when attending critical diseases</i>)
3.	Mbege	Mbege (<i>Traditional beer within Chaga community</i>)
4.	Kigoda	Kigoda (<i>traditional three legged stool used by women in kitchen during cooking, to some community it is used as a royal stool and a stool for seating</i>)

⁷ Maneno yaliyokolezwa ni maneno ambayo yamebeba dhana za kitamaduni katika sentensi hizo

5.	Morani	Morani (<i>youth who serve as warriors in Maasai society</i>)
6.	Laiboni	Laiboni (<i>An old man who heads of the clan in Maasai society</i>)

Chanzo: Matini za Kitalii

Jedwali namba 5 hapo juu linadhihirisha namna mfasiri anavyotumia tafsiri kutimiza lengo la kutafsiri. Kwa kutumia mbinu ya uasilishaji na ufafanuzi wa visawe, mfasiri huweza kutimiza lengo la tafsiri kwa kutoa ufafanuzi wa maneno yenye ujumbe wa kitamaduni. Mbinu hii humsadia hadhira lengwa kuelewa maana na ujumbe wa matini za utamaduni chanzi.

4.2 Utafutaji wa Visawe vya Kitamaduni

Katika hatua hii mfasiri anachunguza na kutafuta visawe vya kitamaduni katika utamaduni wa lugha lengwa vyenye ulinganifu wa maana na ujumbe wa matini ya utamaduni lengwa. Kuna maneno ambayo yamejikita katika utamaduni mahususi na hayaeleweki katika utamaduni mwingine (Micaela, 2008). Utamaduni lengwa unaweza kuwa hauna maneno hayo na viashiria vyake ama vitu vinavyowakilishwa na maneno hayo katika UC vikawa tofauti na vile vinavyowakilishwa na UL. Tofauti hizi zinaweza kuwa katika maana na ujumbe. Kwa maana hiyo, misamiati hiyo huwa imejikita katika utamaduni mahususi na hueleweka kwa watu wa utamaduni huo. Kwa hiyo, huwa ni vigumu kwa watu wa jamii nyingine kuelewa maana na ujumbe wa maneno hayo. Katika hatua hii, mfasiri anatakiwa kubaini misamiati iliyojikita katika utamaduni mahususi wa jamii ili aweze kuikabili misamiati hiyo. Tukirejelea mfano katika jedwali namba 4 hapo juu tunaona kuwa mfasiri amekutana na maneno kama vile 'kinyamkera,' kijumba cha shetani, 'mbege,' Laiboni, morani na 'kigoda.' Maneno hayo yamebeba maana na ujumbe wa kitamaduni, kwa hiyo ni vigumu sana kwa mtu asiye mmoja wa utamaduni huo kuelewa maana na ujumbe wa maneno hayo. Kwa hiyo, ni jukumu la mfasiri kutafuta visawe vya utamaduni katika utamaduni lengwa vinavyofanana na misamiati hiyo ya kitamaduni. Kila utamaduni ni mahususi kwa jamii yake, baadhi ya maneno huweza kuwa na maana katika utamaduni mmoja na yasiwe na maana katika utamaduni mwingine. Kwa hiyo, inapotokea maneno hayo yakawa hayana maana katika utamaduni lengwa ama utamaduni lengwa ukawa hauna utamaduni unaowasilishwa na maneno hayo, mfasiri anatakiwa kuwa makini katika kuteua mbinu ya kuyakabili maneno hayo ili hadhira lengwa iweze kupata maana na ujumbe wa maneno hayo. Mbinu inayofaa ni kuyahamisha maneno hayo kama yalivyo kutoka katika matini lengwa kwenda katika matini chanzi na kuyatolea ufafanuzi wa ziada. Rejea mifano katika jedwali namba 4 hapo juu. Aidha, kuna mambo mawili mfasiri anapaswa

kuyazingatia katika hatua hii; ushirikishaji wa jamii za UC na UL na kuhakiki visawe vya UC na UL.

4.2.1 Ushirikishaji wa jamii za UC na UL

Utafutaji wa visawe ni zoezi ambalo huwa si rahisi hasa kwa misamiati ambayo imejikita katika dhana mahususi za utamaduni wa jamii. Kwa maana hiyo, ili kufanikisha zoezi hili, mfasiri anahitaji kuishirikisha jamii ya utamaduni chanzi na utamaduni lengwa ili aweze kupata visawe vya tamaduni anazozifanyia kazi. Kwa mfano mfasiri anaweza kuwa ni mmilisi wa lugha na utamaduni wa Kiswahili lakini anakutana na neno la kitamaduni katika Kiswahili ambalo hafahamu lina maana gani katika utamaduni wa jamii chanzi itakuwa vigumu kwake kuhawilisha matini hiyo katika utamaduni lengwa. Hivyo, inampasa kushirikisha watu wenye uzoevu na uelewa wa utamaduni wa jamii chanzi na jamii lengwa ili kupata visawe sadifu visivyokuwa na utata wa manaa. Hatua hii itamsaidia mfasiri kupata visawe muafaka vya kitamaduni.

Hatua hii ni muafaka kuzingatiwa na wafasiri wa matini za aina nyingine kama vile; sheria, tiba, sayansi, uhandisi, uhasibu na mahesabu. Mfasiri anapokutana na matini za aina hizo anapaswa kushirikisha wataalamu wa eneo hilo ambao ndio wenye uelewa na ufahamu wa utamaduni huo. Maneno na misamiati ya maneno hueleweka kulingana na utamaduni wa fani inayohusika. Kwa hiyo, mfasiri anapokutana na misamiati wa kisheria anatakiwa ashirikishe wataalamu wa sheria ili kujua dhana hizo, wataalamu wa tiba na madawa, na wataalamu wengine kulingana na misamiati ya fani inayohusika.

4.2.2 Kuhakiki Visawe vya UC na UL

Katika hatua hii mfasiri anatakiwa kufanya uhakiki wa visawe alivyovipata na kupima endapo vinasawiri maana/ujumbe uliokusudiwa katika matini chanzi na matini lengwa. Aidha, mfasiri anatakiwa kujiridhisha kwamba visawe alivyotumia vinawasilisha lengo la tafsiri. kwa kufanya hivyo, mfasiri atafanya ulinganifu wa MC na ML ili kuona kama kuna ulinganifu wa maana na ujumbe wa matini chanzi na kisawe alichokitumia katika matini lengwa. Aidha, hatua hii humsaidia mfasiri kuamua ni kisawe gani kinaweza kutumika kulingana na muktadha wa matumizi ya matini chanzi na matini lengwa. Kwa mfano, baadhi ya maneno hutumika tofauti kulingana na muktadha wa jamii chanzi. Katika data za matini za kitalii baadhi ya maneo yalionekana kutumia visawe zaidi ya kimoja. Tazama mifano ifuatayo hapa chini;

- (i) Kigoda –*royal stool/chair*
- (ii) Kigoda-*three leged stool/chair*

(iii) Kigoda – *traditional stool/chair*

Katika mifano hiyo, mfasiri anaweza kuamua kuteua kisawe kulingana na utamaduni wa jamii chanzi na muktadha wa matumizi wa neno hilo. Kuna jamii ambazo ‘kigoda’ hutumika kama kiti cha kifalme na mfalme anapokufa huzikwa akiwa amekaa katika kiti hicho. Mfano mzuri ni jamii ya Wahehe wa Iringa nchini Tanzania. Endapo utamaduni huu ndio umelengwa kuwasilishwa basi, mfasiri atateua kisawe kinachosawiri maana na ujumbe wa matini chanzi kuwa ni ‘royal chair.’

4.3 Mchakato wa Tafsiri

Mchakato wa tafsiri ni zoezi la kuhawilisha maana na ujumbe wa matini chanzi kwenda katika matini lengwa. Katika muktadha huu, hii ndiyo hatua ya uhawilishaji wa ujumbe wa matini chanzi kwenda katika matini lengwa. Tunaita hatua hii ni mchakato wa tafsiri kwa sababu, hatua hii ndiyo hatua mama ambayo mfasiri anatumia weledi, maarifa na nadharia za tafsiri katika uhawilishaji wa matini aliyonayo. Ni sehemu nyeti na muhimu ambayo inahitaji umakini zaidi katika kuamua visawe vya kutumia kutafsiri matini, mbinu za tafsiri ili kupata tafsiri yenye tija kwa hadhira mahususi. Hapa mfasiri anaweza kutafsiri kwa kutumia mbinu kadha wa kadha ambazo zimebainishwa katika nadharia ya tafsiri. Katika hatua hii mfasiri huhawilisha ujumbe wa lugha ya matini chanzi katika lugha ya matini lengwa kwa kutumia mikakati aliyotumia katika hatua zilizotangulia. Ni katika hatua hii, ambapo mfasiri huamua kutumia mbinu kadha wa kadha za tafsiri ili kupata zao la matini lengwa. Jambo muhimu zaidi ni uhusishaji wa nadharia ambayo mfasiri amebaini kuwa itamfaa katika hatua za awali. Hatua hii ina vipengele viwili yaani; upimaji wa ulinganifu wa visawe vya MC na ML na upimaji wa ushikamani wa UC na UL.

4.3.1 Kupima Ulinganifu wa Visawe vya MC na ML

Zoezi la uhawilishaji wa mawazo huhitaji uwazi na uyaakinifu katika kuhakikisha kuwa kuna ulinganifu wa visawe vya MC na ML. Ulinganifu huu ni katika maana na ujumbe wa matini chanzi na matini lengwa. Aidha, mfasiri anapaswa kufumbata muundo wa matini chanzi ili kuhakikisha hadharishi matini nyingine tofauti na matini chanzi. Baadhi ya maneno huwa na maana zaidi ya moja katika matini chanzi na hivyo mfasiri anapaswa kuteua visawe muafaka vyenye maana na ujumbe sawa na maana na ujumbe asilia. Upimaji wa ulinganifu wa visawe hujiegemeza katika maana na ujumbe. Mfasiri anapaswa kujiuliza je kisawe A nilichotumia kina ulinganifu sawa na msamiati wa awali. Kwa mfano, katika matini za kitamaduni mfasiri anapaswa kupima ulinganifu wa maana ambao umekusudiwa. Je, kisawe kilichotumika katika LL kinasadifu ujumbe ya LC?

Kwa mfano, tazama mifano katika jedwali lifuatalo ambayo ilionekana kuwa tafsiri yake ni matokeo ya matatizo ya uteuzi wa msamiati.

Jedwali Na. 6: Matatizo ya Uteuzi wa Msamiati⁸

Namba	MUC	MUL
1.	Mafiga	<i>Fire place</i>
2.	Ukuta	<i>Main wall</i>
3.	Upawa	<i>Wooden spoon</i>
4.	Ghala	<i>Storage bin</i>
5.	Kiroto	<i>Drinking bucket</i>

Chanzo: Data za Matini za Kitalii (Mei –Oktoba, 2012)

Mifano katika Jedwali namba 6 inaonesha baadhi ya matini za kitamaduni ambazo zilibainika kutafsiriwa kwa kutumia msamiati usiosadifu maana na ujumbe wa matini chanzi. Ukichunguza mifano hiyo utaona kuwa mfasiri hakufanya upimaji wa ulinganifu wa visawe alivyovitumia katika tafsiri yake. Kwa mfano, neno ‘kiroto’ katika mfano namba 5 kutafsiriwa kama ‘*drinking basket*’ halina uamilifu kwa sababu kisawe cha ‘bucket’ katika Kiswahili ni ‘ndoo.’ Je mtu anaweza kutumia ndoo kunywa maji? Mfano mwingine ni neno ‘ukuta’ katika mfano namba 2 kutafsiriwa kama ‘*main wall.*’ Tafsiri hii ina matatizo. Ili iwe sahihi, matini chanzi ilipaswa iwe ‘ukuta mkuu.’ Matokeo haya yanadhihirisha kuwa, tatizo hilo limetokana na ukosefu wa visawe amilifu katika utamaduni lengwa na tatizo la mfasiri kutokuwa na uelewa wa utamaduni lengwa. Endapo mfasiri wa matini hiyo angefuata na kuzingatia hatua bora za tafsiri angeweza kulinganisha visawe alivyotumia na maana anayoibua. Kwa kufanya hivi angeweza kubaini kuwa visawe alivyotumia havina ulinganifu wa maana na ujumbe. Uzingativu wa hatua hii ungemsaidia kufanya uteuzi wa viaswe muafaka kulingana na muktadha na utamaduni wa jamii chanzi na jamii lengwa.

Hatua hii pia inaweza kutumika katika kutafsiri matini za kisayansi, kiufundi na matini za kawaida, habari na maelezo. Endapo mfasiri ataruka hatua hii, matini inaweza kuwa na ama mkengeuko wa maana au kazalisha matini isiyokuwa na ulinganifu wa maana na ujumbe.

4.3.2 Kupima Ushikamani wa Matini ya UC na UL

Kupima ushikamani wa matini chanzi na matini lengwa ni hatua muhimu sana. Matini chanzi na matini lengwa zinahitaji kuwa na ushikamani wa maana na ujumbe ili kuweza kufanikisha mawasiliano. Endapo matini zote mbili zitakosa

⁸ Mifano hii inapatikana katika Jilala (2014)

ushikamani wa maana na ujumbe basi, matini hizo huwa ni matini mbili tofauti. Ni jukumu la mfasiri kuhakikisha anapima ushikamani wa maana na ujumbe wa matini za utamaduni chanzi na utamaduni lengwa.

Ushikamani wa maana na ujumbe wa matini chanzi na matini lengwa. Matini chanzi inaonyesha kuwa na ushikamani wa maana ya matini chanzi na matini lengwa.

Endapo mfasiri atabaini kuwepo na ushikamani wa maana ya matini chanzi na matini lengwa anaweza kukiri kufanikiwa katika shughuli nzima ya tafsiri. Hii ina maana kwamba, ameweza kuhawilisha ujumbe ulio katika matini chanzi kwa kutumia visawe muafaka na sadifu vya utamaduni lengwa.

Hatua hii ni muhimu sana kuzingatiwa na mfasiri wa matini ya aina yoyote ile. Humsaidia mfasiri kupima ushikamani wa matini alizozifanyaia kazi. Kwa maana hiyo, kila matini hupitia hatua hii ili kuona ni jinsi gani mfasiri amefanikiwa katika kulinda na kuhifadhi ushikamani wa maana na ujumbe wa matini chanzi na matini lengwa.

4.4 Uhusiano

Katika hatua hii mfasiri anachunguza uhusiano wa matini zote mbili. Hapa mfasiri anabainisha endapo matini hizi zinafanana ama kutofautiana kwa kusoma na kuipitia mara kadhaa. Hatua hii ina msisitizo wa vipengele viwili, yaani, kupima kufanana kwa dhana, ishara na ujumbe wa UC (MC) na UL (ML) na kupima uhusiano wa ujumbe wa UC na UL katika MC na ML. Lengo la mfasiri katika hatua hii ni kutaka kulinganisha uhusiano wa matini chanzi na matini lengwa ili kujua kama matini hizo zinahusiano wa karibu ama uhusiano wa mbali. Kuna baadhi ya ishara ama dhana za kitamaduni ambazo hazimo wala hazifahamiki katika utamaduni mwingine. Pamoja na kutokuwepo kwa dhana hizo, mfasiri anapoteua visawe anavyovitumia katika tafsiri yake anapaswa kupima kufanana kwa visawe hivyo katika matini zote mbili. Hii itamsaidia kubaini endapo visawe alivyochagua vina uhusiano wa karibu kimaana na kiujumbe au kuona kama visawe hivyo vinaleta maana sawa ama vina maana tofauti. Tazama mifano katika jedwali namba 7 ambayo inaonyesha visawe vyenye matatizo ya uhusiano wa maana na hatimaye kusababisha matatizo katika tafsiri.

Jedwali Na.7: Visawe Vyenye Matatizo ya Maana

Na.	MC	ML
1.	Kata	<i>Water container</i>
2.	Makobazi	<i>Shoes</i>
3.	Upawa	<i>Spoon</i>
4.	Kibuyu	<i>Container</i>

Chanzo: Matini za Kitalii

Katika mifano hiyo, tunaona kuwa mfasiri aliruka hatua ya kuhakiki uhusiano wa maana na ujumbe wa matini ya utamaduni chanzi na matini ya utamaduni lengwa. Tatizo hili lilisababisha atumie visawe ambavyo havina uhusiano. Ili kuwa na uhusiano wa matini zote mbili alipaswa kuwa na tafsiri kama inavyoonekana katiak jedwali namba 8 hapa chini.

Jedwali Na. 8: Visawe vyenye Uhusiano wa Maana na Ujumbe katika MC na ML

Na.	MC	ML
1.	Kata	<i>Ladle</i>
2.	Makobazi	<i>Sandals</i>
3.	Upawa	<i>Steer</i>
4.	Kibuyu	<i>Calabash</i>

Chanzo: Matini za Kitalii

Mifano katika jedwali namba 8 inadhihirisha uhusiano wa maana na ujumbe wa matini chanzi na matini lengwa.

Aidha, kipengele kingine cha kuzingatia katika hatua hii ni kupima uhusiano wa ujumbe wa MC na ML. Katika hatua hii ni muhimu kwa mfasiri kupima endapo tafsiri aliyofanya mfasiri ina uhusiano wa ujumbe baina ya matini chanzi na matini lengwa. Kwa mfano, kuna baadhi ya visawe ambavyo mfasiri anaviteua kwa kutumia uhusiano wa karibu wa maneno na dhima za maneno hayo katika matini zote. Mfasiri hapa anajaribu kupima ni kwa kiasi gani visawe hivyo alivyotumia vinaleta uhusiano wa ujumbe wa matini zote mbili. Hatua hii ni muhimu kwa sababu wafasiri wengi hushindwa kufikia hapo kwa kupima uhusiano wa ujumbe endapo ni uhusiano wa mbali ama uhusiano wa karibu. Tazama mifano ifuatayo;

Hapa mfasiri anaweza kuwa na tafsiri zaidi ya moja na kupima ni tafsiri ipi ina uhusiano wa karibu na matini lengwa. Rejea mifano ya kigoda na tafsiri zake iliyotolewa hapo awali.

Hatua hii inaweza kutumika katika kutafsiri matini nyingine kwa sababu huwezi kufanya tafsiri bila kuchunguza ama kupima uhusiano wa matini zako unazozishughulikia. Kwa hiyo, katika mchakato wa tafsiri ya aina yoyote mfasili hawezi kuepuka hatua hii.

4.5 Uzalishaji wa ML

Uzalishaji wa matini ndiyo hatua ya mwisho ya zoezi la mchakato wa kutafsiri matini. Baada ya kupitia hatua zote za kutafsiri, mfasiri huwa na kazi (ML) ambayo ni zao la matini chanzi. Katika hatua hii, mfasiri huzalisha matini chanzi kwa kuzingatia vigezo na hatua zote alizopitia. Ni katika hatua hii ambapo mfasiri huwa na muswada wa tafsiri ulio katika lugha lengwa. Muswada ambao umetokana na lugha matini ya utamaduni wa lugha chanzi. Ili kuwa na matini iliyo bora na sadifu, mfasiri katika hatua hii hupitia vipengele vingine muhimu kama vile; uhariri, ushirikishaji wa hadhira ya UC na UL, ushirikishaji wa wataalamu wa lugha na tafsiri, urudusu wa rasimu ya kwanza na usawidi wa rasimu ya mwisho. Sehemu ifuatayo inafafanua vipengele hivyo kwa upana wake.

4.5.1 Uhariri

Hiki ni kipengele muhimu cha kuzingatia baada ya kuzalisha matini lengwa. Matini lengwa inapokamilika lazima ifanyiwe uhariri ili kuzalisha matini bora. Uhariri kwa hatua ya kwanza hufanywa na mfasiri mwenyewe kwa kuisoma mara kadhaa matini lengwa. Hatua ya pili ya uhariri ni kumpa msomaji wingine aweze kuisoma na kubainisha matatizo ya matini lengwa. Katika hatua hii inapendekezwa msomaji wa pili apewe matini zote mbili yaani; matini chanzi na matini lengwa. Hatua ya tatu ni mfasiri kuisoma tena kazi yake baada ya kurekebisha matini lengwa kwa kutumia maoni ya msomaji wa pili. Kwa ujumla, uhariri ni hatua muhimu sana na husaidia kuondoa makosa ya maandishi, kurekebisha makosa ya kisarufi, matatizo ya upatanifu wa kisarufi, utata wa maana na ujumbe wa matini. Aidha, kipengele hiki husaidia kuondoa makosa ya kiuchapaji na pia kuweka sentensi au kifungu cha habari kiwe na maana sadifu baina ya matini zote mbili. Kwa mfano, tukirejelea matini za kitalii ilibainika kuwa, tatizo la uhariri ni moja ya tatizo kubwa lililosababisha upungufu wa maana. Tazama mifano katika jedwali namba 7.

Jedwali Na.9: Matini Zenye Makosa ya Kisarufi

Na.	MC	ML
1.	Mfu huzikwa akiwa amekaa kitini na huelekezwa Magharibi Kwetuhumile inakoaminika ni chimbuko la Wahehe	<i>The dead are buried while seated heading west where is believed to be the Hehe origin.</i>
2.	Wahehe wana historia kubwa katika uongozi na utawala.	<i>The Hehe has a long history in leadership and fight experience.</i>

Chanzo: Data za Matini za Kitalii

Mfano katika jedwali namba 9 hapo juu unadhihirisha tatizo la makosa ya kisarufi ambayo yalibainika kuwa yametokana na ukosefu wa ujuzi wa lugha. Mfano, mfasiri ametumia neno 'heading' badala ya neno 'facing' ambalo lingekuwa sahihi katika muundo wa sentensi hiyo. Katika mfano namba 2, kuna tatizo la lugha ya Kiingereza. Matumizi ya neno 'has' ambalo ni mofimu ya umoja wakati katika lugha lengwa ni tofauti na lugha chanzi ambayo imetumia mofimu ya wingi (/wa- /). Kwa maana hiyo matumizi ya mofimu ya wingi yanadhihirisha matatizo ya kimawasiliano na kuondoa ushikamani wa matini chanzi na matini lengwa kimuundo. Katika sentensi hiyo neno sahihi lilikuwa ni 'have' ambalo ni mofimu inayowakilisha wingi.

Data hiyo inadhihirisha kuwa, endapo mfasiri angefanya uhariri wa matini lengwa angeweza kuepuka matatizo hayo ya kimawasiliano. Kwa maana hiyo, hatua hii ni muhimu sana kwa wafasiri wa matini za aina zote. Kipengele hiki kitamsaidia mfasiri kuzalisha matini bora na sadifu isiyo na makosa ya kisarufi na na ya kiuchapaji. Uhariri unaweza kufanyika kwa kusoma mara kadhaa matini chanzi ili kuweza kubaini matatizo yanayojitokeza katika matini lengwa.

4.5.2 Ushirikishaji wa Hadhira ya UC na UL

Katika kipengele hiki mfasiri anatakiwa kuwashirikisha hadhira wa matini zote ili kuona kama matini chanzi imetendewa haki na kuna uaminifu ambao umezingatiwa katika kuzitendea haki tamaduni za matini zote. Kwa mfano, endapo matini lengwa haieleweki kwa hadhira lengwa basi, matini hiyo itakuwa na kasoro amabzo mfasiri anahitaji kuzirekebisha kabla ya kuitoa matini lengwa kama zao la tafsiri.

4.5.3 Ushirikishaji wa Wataalam wa Lugha na Tafsiri

Kipengele hiki ni muhimu kwa mfasiri ambaye kazalisha kazi ya tafsiri. Kabla ya kuitoa kazi hiyo kama toleo la mwisho ni vema ikapitiwa na wataalamu wa lugha

na tafsiri. Hawa watasaidia kubaini makosa mbalimbali na kupendekeza mbinu bora ambayo pengine ingekuwa bora katika kutafsiri matini hizo ili kuleta ushikamani wa maana na ujumbe. Vile vile, watasaidia kukagua na kubaini makosa ya kisarufi, muundo na maana ya maneno kilesksika na kimuktadha. Endapo mfasiri ataruka hatua hii anaweza kuzalisha tafsiri ama yenye mkanganyiko au ukengeufu wa kisarufi na kimaana. Jilala (2014) anadai kuwa, moja ya sababu za matatizo ya mawasiliano katika matini za kitalii ni kutowashirikisha wataalamu wa lugha na tafsiri; vile vile tafsiri za matini za kitalii kufanywa na wafasiri wasio na taaluma ya tafsiri.

4.5.4 Udurusu wa Rasimu ya Kwanza

Hii ni hatua muhimu sana inayosisitizwa na Mwansoko, (1996:21). Udurusu hutoa nfasia ya kwanza ya kuisahihisha matini iliyokwisha tafsiriwa (Mwansoko, 1996). Mwansoko anapendekeza hatua hii ifanyike siku inayofuata baada ya matini kukamilika. Kwa kufanya hivi, mfasiri anaweza kuwa ametulia kiakili na kimwili na hivyo kuifanya kazi yake kwa makini na mawazo mapya. Larson (1984:482) kama alivyonukuliwa na Mwansoko anapendekeza urudusu ufanyike baada ya juma moja ama mawili kufuatia kukamilika kwa rasimu ya kwanza ya tafsiri. Kwa kufanya hivi ataifanya kazi yake akiwa na nguvu mpya na kwa uyakinifu. Kama anavyopendekeza Mwansoko, mfasiri katika hatua hii asome matini yake kwa sauti huku akilenga kurekebisha makosa ya kimsamiati na miundo ya tungo, kuondoa utata wa miundo na matumizi ya visawe, kusahihisha ushikamani wa tungo, mawazo ili kuweka mtiririko mzuri wa tungo, kuchunguza usahihi wa maana kwa kuondoa upanuzi wa maana na ufinyu wa maana unaojitokeza kwenye matini lengwa kwa kufanya ulinganishi na matini chanzi, kuchunguza na kurekebisha lugha iliyotumika katika matini chanzi na kuhakikisha ipo katika uasilia unaokubalika kulingana na miundo na maumbo ya ruwaza ya lugha lengwa, kubaini iwapo maana maana na ujumbe mkuu wa matini chanzi unajitokeza waziwazi katika matini lengwa.

4.5.5 Usawidi wa Rasimu ya Mwisho

Baada ya kazi ya tafsiri kupitia katika hatua hizo zote mfasiri anapaswa kufanya marekebisho yote yaliyojibainisha katika matini chanzi. Maoni na mapendekezo ya mhariri ambaye ameisoma kwa makini matini lengwa anapaswa kuyazingatia na kuyaingiza katika rasimu yake ya mwisho. Aidha kabla hajaitoa rasimu hii kwa mteja wake, mfasiri anatakiwa ajiridhishe kwa kuisoma upya ili kuona hakuna makosa mengine yanayojitokeza katika matini hiyo. Rasimu ya mwisho ndiyo rasimu ambayo itaenda kwa hadhira wa matini lengwa.

Aidha, hatua hii kama inavyopendekezwa na Mwansoko (1996) inafaa na ni muhimu kupitiwa na mfasiri anayetafsiri matini ya aina yoyote ile. Uzingativu wa

hatua hii husaidia kuzalisha matini ambazo ni sadifu na zisizo na makosa ya kihariri, kisarufi, kimaana na kimuundo katika tafsiri.

5. Ufaavu wa Hatua za Kutafsiri Matini za Kitamaduni katika Matini Zingine

Baada ya kupitia na kujadili hatua tano za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala, 2014 na jinsi zinavyoweza kutumika katika zoezi la mchakato wa kutafsiri matini za kitamaduni. Katika mjadala huo, makala haya yamejadili kila hatua na vipengele vyake na kuonyesha jinsi ambavyo mfasiri anapaswa kuvizingatia katika hatua hizo kwa vitendo. Pamoja na mjadala huo, makala haya yameonesha umuhimu wa kuzingatia hatua hizo na matatizo ambayo mfasiri anaweza kuyapata endapo hatazingatia hatua hizo za tafsiri. Swali ambalo makala haya yalikusudia kulijibu ni endapo hatua hizo zinaweza kutumika kutafsiri aina nyingine za matini au hatua hizo ni mahususi kwa matini za kiutamaudni tu? Makala haya yamebaini kuwa, hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala (2014) zinaweza kutumika kama dira ya kutafsiri matini zingine zisizo za kitamaduni. Katika kufafanua na kujadili hatua za tafsiri, mjadala umedhihirisha kuwa, hatua za tafsiri zinafaa na zinaweza kutumika kama dira ya kutafsiri matini za aina zingine kama vile; matini za kiufundi, kifasihi na kisayansi. Sababu inayofanya hatua hizi zionekane kufaa katika kutafsiri matini zingine ni;

- (a) Hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala zimetokana na data za utafiti ambazo zilihusisha wafasiri wa matini za kitalii, wanafunzi wa tafsiri na wataalamu wa tafsiri. Kwa kuhusisha makundi haya, mapendekezo na maoni ya hatua za tafsiri yalitolewa na wadau wa tafsiri. Kwa maana hiyo, hatua hizi zinaweza kuwa ni hatua za jumla katika kutafsiri matini yoyote.
- (b) Hatua hizi zimeunganisha hatua za wataalamu wengine hususani Newmark (1988) na Mwansoko (1996) na kuongeza baadhi ya hatua zilizopendekezwa na wafasiri wa matini za kitamaduni. Uhusishaji wa hatua mbalimbali umesaidia kuzipa nguvu hatua hizi na kuongeza wigo na upana wa mawanda ya utumizi katika mchakato wa tafsiri. Kwa maana hiyo, hatua hizi ni dira mahususi inayoweza kutumika kama mwongozo wa mfasiri katika kuzikabili na kuzitafsiri matini za aina zote na kuzitoa katika umahususi na hivyo matini yoyote inaweza kukabiliwa kwa hatua hizi.
- (c) Matini za tafsiri huingiliana. Hii ina maana kwamba, katika matini ya kifasihi unaweza kubaini maneno ama misamiati ya kiufundi, kitamaduni nk. Kwa maana hiyo, hatua ambazo zinaweza kutumika katika tafsiri ya matini ya aina moja inaweza pia kutumika katika tafsiri ya aina nyingine. Matini huhitaji uwazi na mantiki katika kufikisha maana na ujumbe wa maneno katika matini chanzi na matini lengwa. Kwa maana hiyo, hatua za tafsiri ni nyenzo muhimu katika kufikisha ujumbe na maana sadifu ya

matini. Ni hatua za tafsiri ambazo zinaweza kupotosha ama kudhihirisha maana na ujumbe wa matini chanzi na matini lengwa.

Kutokana na sababu hizo tunaweza kuhitimisha kuwa hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala (2014) zinaweza kutumika kama kiunzi cha kuzikabili matini za aina yoyote ile. Kwa maana hiyo, hatua za tafsiri za jumla zinaweza kuonekana kama zinavyojitokeza katika jedwali namba 10 hapa chini.

Jedwali Na 10: Hatua za Kutafsiri Matini za Kitamaduni

Na.	Hatua	Vipengele vya Kuzingatia.
VI.	Maandalizi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchambua maudhui ya matini • Kubainisha maneno ya kitamaduni • Kubaini ujumbe na maana ya maneno • Kubaini lengo la MC na ML
VII.	Utafutaji wa visawe vya (kitamaduni, kisayansi, kisheria n.k.)	<ul style="list-style-type: none"> • Ushirikishaji wa jamii za MC na ML. • Kuhakiki visawe vya MC na ML.
VIII.	Mchakato wa tafsiri	<ul style="list-style-type: none"> • Kupima ulinganifu wa visawe vya kitamaduni katika MC na ML • Kupima ushikamani wa matini ya MC na ML.
IX.	Uhusiano	<ul style="list-style-type: none"> • Kupima kufanana kwa dhana, ishara na ujumbe wa MC na ML • Kupima uhusiano wa ujumbe wa MC na ML
X.	Uzalishaji wa ML	<ul style="list-style-type: none"> • Uhariri • Ushirikishaji wa hadhira ya MC na ML • Ushirikishaji wa wataalam wa lugha na tafsiri • Udurusu wa rasimu ya kwanza • Usawidi wa rasimu ya mwisho

Hatua za tafsiri katika jedwali hilo, zimerekebisha kutoka katika hatua za Jilala 2014 kwa kuondoa neno utamaduni ili kuzifanya ziwe ni hatua za jumla za kutafsiri matini.

6. Hitimisho

Lengo kuu la makala haya ilikuwa ni kufanya tathimini ya hatua za tafsiri kama nyenzo ya ufanisi wa mawasiliano katika tafsiri. Ili kufikia lengo hilo, makala haya yamefanya ufafanuzi wa hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala, 2014 katika modeli yake ya MMK. Makala haya yamejadili kwa kina kwa kutumia mifano ya matini za kitalii jinsi ambavyo hatua hizo zinafanyika kwa vitendo katika mchakato wa tafsiri. Katika mjadala huo, makala haya pia yanaonesha na kupima ufaavu wa hatua hizo katika kutafsiri matini za aina nyingine. Makala haya yamejadili kuwa ufanisi wa mawasiliano hutgemea uzingativu wa hatua bora za tafsiri ili kuondoa matatizo ya tafsiri. Aidha, makala haya yanahitimisha kuwa, hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala, 2014 zinafaa kutumika katika kutafsiri matini za aina nyingine. Mjadala huu unadhihirisha kuwa, hatua hizo zimegusa vipengele mahususi ambavyo vinazingatia nadharia, weledi na uzoefu katika tafsiri. Makala haya yanajadili kuwa, hatua za tafsiri ni nyenzo mahususi katika ufanisi wa mawasiliano. Endepo mfasiri atakiuka hatua za tafsiri anaweza kuzalisha tafsiri tenge isiyo na usadifu wa maana na ujumbe wa matini chanzi. Hatua za tafsiri ndiyo kiungo kikuu katika zoezi ka tafsiri, ni kiungo ambacho humwongoza mfasiri katika kuteua mbinu muafaka za tafsiri na kuzalisha matini bora zaidi.

Marejeo

- Beaton, E. D., Bombardier, C., Guillemin, F na Ferraz, B. M. (2002). *Guideline for The Process of Cultural Adaptation of Self- Report Measures*. Spine, Juzuu la 25 Na. 24, uk. 3186- 3191.
- Catford, J. C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University.
- House, J. (2009). *Translation*. Oxford: Oxford University Press.
- Jilala, H. (2014). *Athari za Kitamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu (Ph.D Kiswahili) (haijchapishwa)*. University of Dar es Salaam.
- Katani, D. (1999). *Translating Culture: An Introduction for Translators, Interpreters and Mediators*. Manchester: St. Jerome Publishing.
- Lauscher, S. (2000). *Translation Quality Assessment: Where can Theory and Practice meet? The Translator*, Juzuu Na. 6, (2), uk.149-168.

- Micaela, M. (2008). *An Approach to New Trends in Translation and Culture Identity*. Newcastle Upon Tyne, NE6 2XX, UK: Cambridge Scholars Publishing 12 Back Chapman Street.
- Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies. Theories and Application*. London: Routledge.
- Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*. London: Prentice Hall.
- Nida, E. A. (1975). *Componential Analysis of Meaning. An Introduction to Semantic Structures*. Paris: Mouton.
- _____ (1964). *Towards a science of Translating*. Leiden: EJ. Brill.
- _____ (2001). *Language and Culture: Context in Translating*. Shanghai: Shanghai Foreign Language Ed Press.
- Nida, E. A. and Taber, C. (1969). *Theory and Practice of Translating*. Leiden: Brill.
- Nord, C. (2001). *Translating as A Purposeful Activity: Functionalist Approaches Explained*. Manchester: St. Jerome Publishing.
- Vermeer, H. (1989). Skopos and Commission in Translational Activity. Katika Venuti, L. (Mh.). *The Translation Studies Reader*. London: Routledge.
- Venuti, L. (2002). *On The Different Methods of Translating*. The Translation Studies reader.
- Wang, L. (2008). *Cultural Transfer in Legal Translation: A Case Study of The Translation of The Common Law in Chinese*. Hong Kong: City University of Hong Kong.